Mkombozi
Empower. Engage. Enable.

TOLEO FUPI

Sensa ya watoto na vijana walioko mitaani Moshi na Arusha 2010

Written by: Katie Bunten-Wren
Edited by: William Raj, Turid Misje and Katie Bunten-Wren

I. Muhtasari

■ Sensa ya Mkombozi ya mwaka 2010 juu ya watoto na vijana walioko mitaani ililenga kupata na kutathmini takwimu za idadi ya watoto na vijana wanaokaa au kufanya kazi mitaani katika manispaa ya Moshi na Arusha.
■ Sensa ilifanyika kwa masaa 12 kila mji kukiwa na timu ya wahojaji waliokuwa wakiwafikia watoto na vijana wakiwa na madodoso yalikuwa na maswali juu ya umri, jinsia, kujihusisha kwao na maisha ya mtaani, walikotokea, elimu na shughuli zao za kila siku.
■ Matokeo ya awali ya sensa yalionyesha kwamba kulikuwa na ongezeko la +17% kwa walioko mtaani muda wote na kupungua kwa -4% kwa walioko mtaani kwa muda. Kwa Arusha, kulionekana kupungua kwa makundi yote, walioko muda wote na walioko kwa muda tu, wakati ambapo kwa Moshi ilionekana kulikuwa na ongezeko la watoto walioko mtaani kwa muda na zaidi hasa ongezeko kubwa kwa wale walioko mtaani muda wote.
■ Kwa ujumla, watoto na vijana 1,108 walitambuliwa kama wanaojihusisha na shughuli za mtaani kwa miji ya Moshi na Arusha; kati yao 466 wanaokaa mtaani kwa muda na 122 wanaokaa mtaani muda wote Moshi, na 381 wanaokaa mtaani kwa muda na 139 wanaokaa mtaani muda wote Arusha.
■ Pia ilionekana dhahiri kwamba toka mwaka 2006 hakukuwepo ongezeko la watoto na vijana walioko mitaani kutokea kwenye jamii lengwa za Mkombozi, ila kusema ukweli kuna kupungua kwa kila moja katika hizo jamii.

II. Ufafanuzi Muhimu

■ Walioko/Wanaokaa/Wanajihusisha mitaani: Mkombozi haitumii tena dhana ya "watoto wa mitaani", kutokana na kutambua ukweli kwamba "Mitaa haizai watoto bali watu ndio huzaa watoto" ila kutokana na fikra potofu na uwezekano wa kunyanyapaa njia hii ya kuwapachika watoto majina inaweza kuhalalishwa. Badala yake, dhana ya "watoto na vijana walioko/wanaokaa/wanajihusisha mitaani" inatumika.
■ Muda wote: Kwa madhumuni ya ripoti hii, kujihusisha mtaani muda wote kuna maana ya wale watoto na vijana ambao walijibu "Ndiyo" kwa swali hili "Unashinda kutwa na kulala mtaani usiku?"
■ Kwa Muda: Kwa madhumuni ya ripoti hii, kujihusisha mtaani kwa muda kuna maana ya wale watoto na vijana ambao walijibu "Ndiyo" kwa swali hili "Unafanya kazi, au kuomba au kutumia muda wako mtaani mchana na kurejea nyumbani usiku?"

- Sensa badala ya Uchunguzi: Mkombozi imechagua kuliita zoezi hili sensa kwa sababu tulikusudia, kwa kuzingatia ufinyu fulani, kuwahesabu watoto na vijana wote walioko mitaani Moshi na Arusha.
- Ushiriki wa Jamii: Kusaidia, kushirikisha na kuwezesha jamii kuchukua jukumu kubwa zaidi la kuhakikisha watoto wanakua vyema katika mazingira salama na waweze kushiriki katika maendeleo yao wenyewe.

III. Demografia

- Watoto na vijana 1,373 walihojiwa Moshi na Arusha. Kati ya hao waliohojiwa, 81% (1,108) walitambuliwa kuwa wanajihusisha na maisha ya mitaani.
- Moshi, 588 walitambuliwa kama wanaojishughulisha mitaani; 466 wanaojihusisha mitaani kwa muda na 122 wanaokaa mtaani muda wote. Kulikuwepo na ongezeko kwa wote, wanaokaa mtaani kwa muda na wanaokaa muda wote toka mwaka 2006 mjini Moshi.
- Kwa Arusha, watoto na vijana 520 walitambuliwa kuwa wanaojihusisha mtaani; 381 wanaokaa mtaani kwa muda na 139 wanaokaa muda wote. Hii ilionyesha kupungua kwa wote, wanaokaa mtaani kwa muda na wale wanaokaa muda wote toka mwaka 2006 katika mji wa Arusha.
- 65% ya watoto na vijana wanaokaa mitaani wako ndani ya makundi lengwa yetu kwa kuwa wana umri wa chini ya miaka 18.
- Mwaka 2006, 10% ya watoto na vijana wa muda wote na 16% ya wanaokaa mitaani kwa muda walikuwa wakike. Kwa ujumla, ni 2% tu ya wanaokaa mtaani muda wote ni watoto wakike, wakati ambapo 13% ya wanaokaa mtaani kwa muda tu ni watoto na vijana wakike. Katika hao watoto na vijana wakike, wengi wao walitaja ngono au ukahaba kama mojawapo ya kazi zao za kila siku.

IV. Mwelekeo Kijiografia

- Kutoka 2006 hadi 2010 kumekuwepo kupungua kwa watoto na vijana walioko mitaani katika jamii zote lengwa za zamani za Mkombozi.
- Sensa ya mwaka 2010 ilizitambua jamii zifuatazo na maeneo yafuatayo kwa umuhimu idadi kubwa ya watoto na vijana waliosema wanaishi au waliishi huko kabla ya kwenda mtaani: Arusha: Kaloleni (n.26), Levolosi (n. 23), Sokon One (n. 21); Moshi: Kaloleni (n. 54), Soweto (n. 34), Bondeni (n. 26).
- Kwa ujumla, idadi kubwa ya watoto na vijana wote wanaokaa mitaani walitokea Mikoa ya Kilimanjaro na Arusha. Kati ya watoto na vijana wote wanaokaa mitaani Moshi, 73% wanatoka katika mkoa mkubwa wa Kilimanjaro. Hata hivyo, ni 51% ya watoto na vijana wote wanaokaa mitaani wanatoka mkoa wa Arusha.
- Katika ngazi ya wilaya, 56% ya vijana na watoto wanaokaa mitaani walitokea Moshi mjini au Wilaya ya Moshi vijijini wakati ambapo 46% ya wale wa Arusha wanatokea Arusha au wilaya ya Arumeru. Katika ngazi ya kata, maeneo yaliyoongoza Moshi ni Njoro, Pasua na Kaloleni wakati ambapo maeneo yaliyoongoza Arusha yalikuwa Ngarenaro na Unga Ltd.
- Idadi ya watoto na vijana wanaotokea jamii za mijini bado ni ndogo kuliko wale waliosema walikuwa wanaishi maeneo ya mjini kabla ya kuja mitaani. Hii inaashiria kwamba baadhi ya watoto wanaondoka katika jamii zao za asili na kuja kuishi mijini, pengine wakiishi na familia zao, na hatimaye huvutwa kuishi mitaani.

V. Kazi na Elimu

- 88% ya watoto na vijana wote wanaokaa mitaani Moshi na Arusha walisema kwamba walisoma au wanasoma shule ya msingi. Kati ya hao, 20% ni walioacha shule wakati 58% walionyesha wamemaliza shule ya msingi.
- Kulikuwa na uwezekano mkubwa kwa wale wanaokaa mitaani kwa muda, wawe walisoma au wanasoma shule ya msingi na zaidi kwamba wawe wamehitimu elimu ya msingi. Kati ya wale wanaokaa mitaani kwa muda, takriban wote walisema walisoma au wanasoma shule ya msingi. Kwa sasa ukilinganisha na idadi ndogo zaidi ya wale wanaokaa mitaani muda wote. Pia, kulikuwepo na uwezekano mkubwa kwa wale wanaokaa mitaani muda wote kuacha shule kuliko wale wanaoshinda mtaani kutwa tu.
- Shule ambazo watoto na vijana walisema walisoma au wanasoma ndizo zilizoko zaidi katika kata zile zile ambazo zina idadi kubwa ya watoto na vijana wanaokimbilia mitaani. Mjini Moshi, kata maarufu zenye hizo shule zilikuwa Pasua, Kaloleni na Njoro. Kwa Arusha, kata maarufu zenye hizo shule zilikuwa Unga Ltd na Ngarenaro.
- Shughuli za kawaida za kila siku zilizoripotiwa na vijana wa zaidi ya miaka 18 ni kupata mahitaji ya msingi, kufanya kazi na kutumia madawa ya kulevya wakati kwa walioko na umri wa chini ya miaka 18 shughuli za kawaida za kila siku ni kufanya kazi, kucheza na kuomba.
- Kucheza kuliripotiwa zaidi kama shughuli ya kila siku kwa Moshi kuliko Arusha jambo ambalo liliweza kutokana na asilimia kubwa kidogo ya watoto kuwa na umri wa chini ya miaka 18 kuwa Moshi.
- Kutumia na kuuza madawa ya kulevya kulionekana kuwa chini lakini inawezekana kwamba iliripotiwa kwa kiwango cha chini/haikuripotiwa hali ilivyo kuwa kwa watoto na vijana walihofia kupata adhabu kutokana na kufanya shughuli haramu au isiyo haramu endapo wangeripoti shughuli kama hizo. Walio wengi zaidi wana umri wa zaidi ya miaka 15.

VI. Huduma

- Majibu 5 ya kawaida zaidi kwa watoto na vijana walioko mitaani kwa swali lililouliza kuhusiana na huduma gani ambazo wanafikiri mashirika ya yasiyo ya kiserikali pamoja na serikali iwapatie yalikuwa: elimu, msaada wa biashara, ajira, matibabu na malazi.
- Kwa upande wa umri, 76% ya watoto na vijana waliosema elimu ni huduma ambayo wangependa walikuwa na umri wa chini ya miaka 18. Hata hivyo, 58% ya watoto na vijana walisema wangependa msaada wa biashara, na 54% wale waliosema wanataka ajira, walikuwa na umri zaidi ya miaka 18.
- Ni 12% tu ya watoto na vijana walioko mitaani Moshi na Arusha walioonyesha kwamba waliwahi kupata huduma toka Mkombozi. Hata hivyo, inawezekana swali hili halikueleweka kwa kuwa idadi hii haiendani na takwimu zetu za kazi za mitaani.